**TAARIFA FUPI KUHUSU TASAF III MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia TASAF III ulianza rasmi katika Manispaa ya Musoma tarehe **15/07/2014.** Madhumuni ya Mpango huu ni kuziwezesha kaya masikini kupata mahitaji ya msingi na fursa za kujiongezea kipato na kuweka akiba. Wlengwa wa Mpango huu ni kaya masikini katika jamiikwa maeneo ya utekelezaji yaliyoainishwa. Mpango huu ni wa miaka **10** kwa awamu mbili za miaka mitano mitano.

## 1.1 MAELEZO MAFUPI KUHUSU MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI – TASAF III

TASAF awamu ya tatu ni Mpango wa kuziwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu.

Malengo ya Mpango yatafikiwa kwa kufanya yafuatayo:

1) Kutoa ruzuku kwa kaya maskini sana kupata huduma za elimu na afya
2) Kutoa ajira za muda kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi wakati wa majanga mbalimbali mfano ukame, mafuriko n.k
3) Kuboresha maisha na kuongeza kipato kwa wananchi maskini kupitia uwekaji akiba na shughuli za kiuchumi.
4) Kujenga na kuboresha miundo mbinu inayolenga maeneo mahsusi katika sekta za elimu, afya na maji.
5) Kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo katika ngazi zote za utekelezaji.

## 2.0 UTAMBUZI WA KAYA MASKINI

Utambuzi wa kaya maskini ulizingatia kaya ambayo ina hali duni ya maisha ikilinganishwa na kaya nyingine katika jamii. Kaya yenye hali duni ina sifa zifuatazo:

i) Haimudu milo mitatu kwa siku
ii) Ina makazi duni
iii) Ina watoto wanaosoma katika hali duni, hawajaandikishwa au wameacha shule kwa kukosa mahitaji muhimu ya shule kama sare za shule na madaftari
iv) Ina watoto na wajawazito ambao hawaendi kliniki kupata huduma za afya

## 3.0 NAMNA WALENGWA WA MPANGO WALIVYOPATIKANA

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilipitia hatua zifuatazo ili kuwapata walengwa wa Mpango.

1. TASAF III Makao Makuu ilichagua maeneo ya utekelezaji ndani ya Manispaa kutokana na takwimu za viwango vya umaskini ambapo mitaa **30** katika kata **11** ilichaguliwa yenye jumla ya kaya **4,340.**

2.Vikao vya wananchi katika maeneo husika viliitishwa na kuchagua kaya maskini sana ambazo zinakidhi vigezo vya kusaidiwa wakiongozwa na wawezeshaji wa Mpango, jumla ya kaya 4,095 zilitambuliwa .
3. Majina ya walengwa yaliyopendekezwa yaliwasilishwa TASAF Makao Makuu na kuchujwa kupitia mfumo wa kompyuta na kubaki na wale tu waliokidhi vigezo vya kuwa kwenye Mpango yenye jumla ya kaya **3,065.**
4. Majina ya walengwa waliokidhi vigezo yaliwasilishwa katika maeneo husika na kufanyiwa uhakiki wa mwisho na jamii husika kwa kushirikiana na wawezeshaji wa Mpango wa kunusuru kaya maskini chini ya usimamizi wa viongozi wa serikali za mitaa ambapo jumla ya kaya **2,719** zilikidhi vigezo vya kuwa walengwa katika Mpango huu wa kunusuru kaya maskini.
5. Wakati zoezi la uhawilishaji fedha linaendelea kwa kaya masikini ilibainika kuna kaya ambazo hazikuwa na sifa hivyo ziliondolewa na kubaki na kaya **2422**

## 3.1 MCHAKATO WA MALIPO KWA KAYA MASKINI

Ni kupeleka fedha za Mpango kwa walengwa kila baada ya miezi miwili**(2)**
Fedha hii inatolewa katika makundi mawili

1. Ruzuku ya Msingi
2. Ruzuku ya Masharti

### 1. RUZUKU YA MSINGI

Hii ni ruzuku isiyo na masharti hutolewa kwa kaya zote ambazo zimetambuliwa kuwa ni maskini kwa mwezi ni Tshs.10,000/= kwa miezi miwili ni Tshs.20,000/=

### 2. RUZUKU YA MASHARTI

- Hii ni ruzuku yenye masharti hutolewa kwa kaya maskini yenye mama wajawazito atakayehudhuria kliniki mara 4 kabla ya kujifungua na kupata mafunzo elekezi ya Afya na lishe
- Kaya yenye watoto chini ya miaka 0-5 kwa mwezi ni Tshs.2,000/= kwa miezi miwili ni Tshs.4,000/= atakayehudhuria kwenye kliniki mara 1 kwa mwezi na kupata mafunzo elekezi ya Afya na lishe.
- Kaya yenye watoto wenye umri wa miaka 6 - 13 wa shule za msingi watakaohudhuria masomo darasani kwa 100% au 80% kwa sababu za msingi kama ugonjwa,kufiwa n.k. ni Tshs. 4,000/= kwa kila mmoja hivyo kwa miezi miwili ni Tshs.8,000/=
- Kaya yenye wanafunzi wa sekondari miaka 14 - 17 Elimu ya sekondari kidato 1- 4 (O level) wanaohudhuria masomo kila siku 100% au 80% kwa sababu za msingi kama ugonjwa,kufiwa n.k. kila mwezi Tshs. 4,000/= kwa kila mmoja hivyo kwa miezi miwili ni Tshs.8,000/=
- Kaya yenye wanafunzi wa sekondari kidato 5-6 (A level) wanaohudhuria masomo kwa 100% au 80% kwa sababu za msingi kama vile ugonjwa,kufiwa n.k. kila ni Tshs. 6,000/= kwa kila mmoja hivyo kwa miezi miwili ni Tshs. 12,000/=

## 3.2 UHAKIKI WA HUDUMA ZA ELIMU NA AFYA

Uhakiki wa utimizaji wa masharti ndio njia halisi ya kufanya Ruzuku kuwa sehemu ya motisha kwa maendeleo ya jamii, pia ni nguzo kuu ya kuwekeza katika rasilimali watu. Kwa hiyo mchakato huu huisukuma kaya kutimiza masharti ili kuweza kupata ruzuku ya masharti mbali na ile isiyo na masharti.

Masharti hayo yasipotekelezwa kaya hiyo hufutiwa ruzuku ya masharti ikiwa fomu zao za Elimu na Afya zitaonyesha kutohudhuria bila sababu za msingi shuleni ama kituo cha afya.

## **3**.3**. UHAKIKI WA MAHUDHURIO NA UKUSANYAJI WA FOMU**

- Walimu huorodhesha wanafunzi ambao hawakuhudhuria shule bila sababu za msingi kwa miezi miwili kupitia fomu za mahudhurio zinazopelekwa shuleni.
- Wahudumu wa Afya watoto wenye umri 0- 5 ambao hawakuhudhuria kliniki kwa miezi miwili kupitia fomu za mahudhurio zinazopelekwa kwenye kituo cha Afya.
- Wahudumu wa Afya huorodhesha mama wajawazito ambao hawakuhudhuria kliniki kwa kipindi cha miezi 4 kabla ya kujifungua (March,April,Sept na Oct)
- Wakuu wa shule, walimu wakuu na waganga wakuu watahakikisha fomu hizo zinakamilika na kurudishwa kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa kisha kwa Mratibu wa Mpango Manispaa ili kutumwa TASAF Makao Makuu.

## **4.0 AJIRA YA MPANGO WA TASAF III**

Kuzisaidia kaya maskini kuweza kuondokana na hali ya umaskini ndani ya miaka mitatu **(3)** ya Mpango wataalam wanaweza kusaidia mchakato huu kwa

- Kutoa Elimu kwa walengwa kuhusu matumizi ya fedha wanazozipata, kupanga bajeti, kuanzisha miradi midogo midogo na kuweka Akiba.
- A/ Maendeleo ya jamii kuwaelimisha wajiunge na vikundi au vikoba
- A/ Kilimo , kuelimisha kuhusu kilimo cha bustani na mboga mboga.
- A/Mifugo kutoa elimu ya ufugaji wa kuku.
- A/Afya kuwaelimisha/ kuwahamasisha wajiunge na mfuko wa Afya ya jamii **CHF** ili kuokoa fedha kwa kutibiwa kila wanapougua.
- Walimu na wazazi kuwahimiza watoto kwenda shule bila kukosa na kupata matokeoa chanya kwa maendeleo ya Taifa.
- Wauguzi na waganga kuwahimiza wajawazito na watoto chini ya miaka 0-5 kuhudhuria kliniki tutakuwa na Taifa lenye watu wenye afya bora kwa maendeleo ya nchi na kuondokana na umaskini unadumaza maendeleo ya Taifa.

### **4.1 WAJIBU WA WAJUMBE WA KAMATI INAYOHUSIKA MA MALIPO (CMCs)**

- Kuwakumbusha wakuu wa kaya kabla ya tukio la malipo na mambo yanayohitajika ili kupokea Ruzuku.
- Utaratibu wa kurudisha kaya upya ,madai na malalamiko yanayoweza kuwasilishwa
- Kuwasaidia kujaza fomu za malalamiko.
- Kuwakumbusha wanakaya kuhusu urekebishaji wa taarifa za kaya mfano. Kuzaliwa mtoto,kifo, kuhama, kuhamia, kuanza shule n.k.

- Kuelimisha walengwa kuhusu tukio la uandikishaji mara ya pili baada ya wawakilishi wa kaya kushindwa kuhudhuria, uandikishaji wa kwanza.

## 5.0 MATOKEO TARAJIWA YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI

1. Kupungua kwa umaskini 52%
2. Kupungua kwa pengo la umaskini 43%
3. Kaya kujiongezea kipato na kuweka akiba
4. Rasilimali watu hasa watoto kujengeka
5. Kupungua kwa utapiamlo
6. Kaya kuwa na rasilimali

## 5.1 MAFANIKIO YA MPANGO TASAF III

1. Kuna mabadiliko makubwa kwa kaya ambazo zimepata ruzuku hizi kwani zipo kaya ambazo zimeanza shughuli za ujasiriamali kama kilimo,ufugaji wa kuku,kuunda vikundi vya ujasiriamali na uanzishaji wa biashara ndogondogo
2. Zipo kaya zimejiunga na mfuko wa Afya wa jamii (CHF) kaya **752** kati **2720** wamejiunga.
3. Watoto kuhudhuria shule wanaotakiwa kuhudhuria kliniki wanahudhuria baada ya kupata ruzuku.

Beatrice Marco
**MRATIBU WA MPANGO**
**TASAF – MANISPAA YA MUSOMA**

**ORODHA YA MITAA NA KATA AMBAZO ZINATEKELEZA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI KATIKA MANISPAA YA MUSOMA**

| NA. | JINA LA KATA | JINA LA MTAA | IDADI YA KAYA ZINAZOHUDUMIWA |
|---|---|---|---|
| 1. | BWERI | 1.NYABISARE | 81 |
| | | 2.NYARUSURYA | 61 |
| | | 3.MACHINJIONI | 88 |
| | | 4.RWAMLIMI | 73 |
| 2. | MAKOKO | 1.NYAMIONGO | 121 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 2.KINYANG'ENA | 55 |
| 3. | MWISENGE | 1.MKINYERERO | 123 |
| | | 2.PWANI | 95 |
| 4. | KIGERA | 1.KWANGWA | 140 |
| | | 2.BONDE KATI | 145 |
| | | 3.MWIYALE | 58 |
| 5. | NYAMATARE | 1.NYABURANGI | 73 |
| | | 2.WAKARA | 70 |
| 6. | NYAKATO | 1.BARUTI | 137 |
| | | 2.MAZIWA | 93 |
| | | 3.BONDENI | 121 |
| | | 4.MLIMANI | 87 |
| | | 5.SAANANE | 112 |
| | | 6.MSHIKAMANO | 171 |
| 7. | KAMUNYONGE | 1.MAJITA ROAD | 33 |
| 8. | NYASHO | 1.NYASHO MAGEREZA | 74 |
| | | 2.NYASHO SOKONI | 63 |
| | | 3.NYASHO M/MMOJA | 35 |
| 9. | KITAJI | 1.KITAJI 'A' | 29 |
| | | 2.KITAJI 'B' | 36 |
| | | 3.KITAJI 'C' | 58 |
| | | 4.KITAJI 'D' | 75 |
| 10. | IRINGO | 1.IRINGO 'A' | 57 |
| | | 2.IRINGO 'C' | 46 |
| 11. | MWIGOBERO | 1.MWIGOBERO 'B' | 12 |
| **JUMLA KUU** | | **30** | **2,422** |